JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Mkuu wa TAKUKURU (M) Kinondoni,
S.L.P 90397, Kinondoni
Simu : 222170852 Nukushi 2170963
Barua pepe: rbckinondoni@pccb.go.tz
Wavuti www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

TAKUKURU KINONDONI, 09/01/2020

UDHIBITI WAFANYIKA KATIKA MIRADI YA MAENDELEO YENYE THAMANI YA BILIONI 12,217,537,000/= KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA HADI DISEMBA, 2019

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni kwa kipindi cha miezi mitatu (3) kuanzia Oktoba 2019 hadi Disemba 2019 imeendelea kutekeleza majukumu yake ya utendaji kazi kama yalivyoainishwa kwenye Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na 11/2007 ambayo yametajwa kuwa ni uelimishaji umma, utafiti na udhibiti pamoja na uchunguzi.

Katika kipindi tajwa juhudi kubwa ilielekezwa katika kudhibiti vitendo vya rushwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika tarehe 24/10/2019 kwa kuhakikisha wananchi wanapata elimu kuhusu madhara ya rushwa katika uchaguzi na umuhimu wa kuchagua viongozi waadilifu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Katika kipindi hiki pia juhudi kubwa ilielekezwa katika kudhibiti vitendo vya rushwa katika miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa katika Manispaa ya Kinondoni na Ubungo. Katika kutekeleza hilo TAKUKURU mkoa wa Kinondoni imekagua na kuhakiki miradi ya maendeleo tisa **(9)** yenye thamani ya Sh. **12,217,537,000/=** na kubaini kuwa kati ya miradi iliyokaguliwa mradi mmoja **(1)** wenye thamani ya **Sh. 86,600, 000/=**una viashiria vya rushwa.

Mchanganuo wa kazi hizo pamoja na nyingine zilizofanyika katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba 2019 ni kama ifuatavyo:-

UFUATILIAJI MIRADI YA MAENDELEO

Mojawapo ya majukumu ya TAKUKURU ni kufuatilia matumizi ya fedha za Umma katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo (Public Expenditure Tracking System). Lengo kuu ni kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa kiwango kinachotakiwa na thamani ya fedha iliyokusudiwa inapatikana. Ufuatiliaji huu husaidia kubaini na kuzuia mianya ya rushwa katika hatua za awali za utekelezaji wa miradi hiyo ili kuzuia upotevu wa rasilimali ambao ungeweza kutokea endapo mianya hiyo haikuzibwa mapema. Mianya hiyo ya rushwa ni pamoja na ucheleweshaji katika kutekeleza miradi, uchepushaji na ufujaji wa fedha za miradi, na kukosekana kwa ushirikishwaji wa wananchi au wadau. Ufuatiliaji unapobaini kuwepo kwa mianya hiyo hatua za haraka huchukuliwa ili kuziba mianya hiyo.

Hatua zinazoweza kuchukuliwa zinajumuisha kuanzisha uchunguzi, kutoa elimu kwa umma na kufanya uchambuzi wa mifumo. Ufuatiliaji huu hufanyika kwa kuangalia utaratibu wa mtiririko wa fedha kutoka chanzo (Hazina, Wafadhili au Vyanzo vya ndani) mpaka kwenye mradi husika (utekelezaji wa mradi) ili kubaini kama kuna mapungufu yaliyotajwa hapo juu.

Katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba 2019 jumla ya miradi ya maendeleo tisa (**09)** ilifuatiliwa ambayo inajumuisha :-

1. Ujenzi wa Soko la Magomeni lenye thamani ya shilingi **Sh. 9,000,000,000/=**
2. Ujenzi wa Zahanati ya Mbopo **Sh. 157,000,000/=**
3. Ujenzi wa kalvati mbili barabara ya Tanganyika na Msigani **Sh. 606, 000,000/=**
4. Ufuatiliaji wa mradi wa ujenzi boksi calavat yenye midomo 4 eneo la Kibamba mji mpya Manispaa ya Ubungo **Sh. 349,365,000/=**
5. Ufuatiliaji wa mradi wa ujenzi wa boksi calavat midomo 2 eneo la Msumi Manispaa ya Ubungo **Sh. 326,407,000/=**
6. Ufuatiliaji wa ujenzi wa kivuko cha waenda kwa miguu eneo la Kibungobungo, barabara ya Msewe Golani, Saranga, Sisi kwa sisi, ujenzi wa kivuko cha miguu Msewe Maji soda na matengenezo ya barabara ya Bush **Sh. 154,665,000/=**
7. Ujenzi madarasa na stoo shule ya msingi Msigani **Sh. 37,500,000/=**
8. Kufuatilia mradi wa ujenzi wa madarasa 4 na matundu 6 ya vyoo ya shule ya msingi Luguruni **Sh. 86,600, 000/=**
9. Kufuatilia ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Ubungo Sh. **1,500,000,000/=**

Kati ya miradi **09** iliyokaguliwa imebainika kuwa mradi **1** wenye thamani ya Sh. **86,600,000/=** taratibu za manunuzi na utekelezaji wa miradi hiyo zilikiukwa na hivyo kubaini kuwepo kwa viashiria vya vitendo vya rushwa. Mradi uliobainika

kuwa na viashiria vya Rushwa ni na ujenzi wa madarasa 4 na matundu 6 ya vyoo ya shule ya msingi Luguruni wenye thamani ya **Sh. 86,600, 000/=**

Pia katika miradi mingine 08 yenye thamani ya shilingi **12,130,370,000/=** ufuatiliaji umebaini kuwepo ucheleweshwaji katika utekezaji wake na hivyo kuzishauri mamlaka husika na kwa sasa ujenzi unaendelea vizuri.

TAKUKURU mkoa wa Kinondoni imechukua hatua ya kuanzisha uchunguzi kwa mradi mmoja uliobainika kuwepo ukiukaji kwa taratibu kwa lengo la kujua sababu za ukikwaji huo na pale itakapothibitika kuwa kuna vitendo vya rushwa vimetendeka hatua stahiki zitachukuliwa. Aidha katika kipindi tajwa uchambuzi wa mifumo **2** umefanyika, Warsha **5** zimefanyika na maazimio **5** yamewekwa kwa lengo la kuziba mianya ya Rushwa iliyojitokeza.

ELIMU KWA UMMA

TAKUKURU ina jukumu la msingi la kuelimisha umma wa watanzania ili washiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa kwa lengo la kuifanya jamii ielewe kuwa mapambano dhidi ya rushwa sio la Serikali pekee bali ni jukumu la kila mwananchi kushiriki kikamilifu katika vita hii kwa kutotoa wala kupokea rushwa.

Katika kutekeleza jukumu hili njia mbalimbali hutumika kama vile semina, vipindi vya redio, uandishi wa Makala, mikutano ya hadhara, maonyesho, ufunguaji na uimarishaji wa klabu za wapinga rushwa katika vyuo, shule za sekondari na shule za msingi.

Katika kipindi cha Oktoba, 2019 hadi Disemba, 2019, Klabu za wapinga rushwa **212** zimefunguliwa na klabu **107** zimeimarishwa katika shule za Msingi, Sekondari na vyuo. Lengo ni kuwapa uelewa wanavyuo na wanafunzi ambao ni wanachama wa klabu hizo juu ya sababu, madhara ya rushwa na mbinu za kupambana nayo kwa lengo la kuwajenga katika misingi ya uadilifu ili waichukie rushwa wakiwa wadogo na kuwaandaa kuwa watumishi na viongozi waadilifu pindi watakapopewa dhamana katika ofisi mbalimbali.

Katika kipindi hicho TAKUKURU (M) Kinondoni iliweza kutoa Semina **32** kwa Watumishi wa kampuni ya ulinzi ya SGA, Wasimamizi wa mtihani wa Taifa wa darasa la nne, Watumishi wa TRA, Watumishi wa TANESCO, Watumishi wa COSOTA, Polisi, Watumishi wa Mahakama, Wasimamizi wa Uchaguzi wa

serikali za Mitaa, Wakuu wa Idara, watendaji wa kata na mitaa, wenyeviti na wajumbe wapya wa mitaa waliochaguliwa na wanachama wa vicoba endelevu.

Aidha, jumla mikutano ya hadhara **92** ilifanyika kwa wananchi mbalimbali ikiwa ni pamoja na madereva wa Daladala, Bodaboda, na Bajaji ambapo walipata elimu ya madhara ya rushwa katika uchaguzi, na matumizi ya TAKUKURU App katika kutoa taarifa za vitendo vya rushwa barabarani kupitia kampeni ya UTATU. Pia vipindi **2** vya Televisheni na Redio vilirushwa kwa lengo la kutoa elimu ya madhara ya rushwa na jinsi ya kupambana na rushwa katika jamii na zaidi ya wananchi **10,000,000** walinufaika na elimu hiyo.

UCHUNGUZI

Jukumu la Tatu la TAKUKURU ni kufanya uchunguzi wa makosa yote yaliyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na kupambana na Rushwa namba 11/2007 na hatimaye kuwafikisha watuhumiwa mahakamani na kuendesha kesi zote zinazohusiana na makosa ya rushwa.

Kwa mwezi Oktoba, 2019 hadi Disemba, 2019 TAKUKURU (M) Kinondoni ilipokea taarifa mpya **174** kutoka kwa wadau ambao ni vyombo vya habari, vyombo vya ulinzi na usalama, Idara na Taasisi mbalimbali pamoja na watu binafsi. Majalada mapya ya uchunguzi **13** yalifunguliwa katika kipindi tajwa kwa ajili ya uchunguzi wa kina na uchunguzi wa majalada **89** yaliyofunguliwa kipindi cha nyuma uliendelea. Katika kipindi tajwa Jamhuri ilifungua kesi mpya **06** na kesi nyingine **06** zilizomalizika kusikilizwa Jamhuri imeshinda. Mkoa uliendelea kuendesha jumla kesi **23** ambazo zipo katika hatua mbalimbali

Katika kipindi cha Oktoba, 2019 hadi Disemba, 2019 idara zilizoongoza kwa kulalamikiwa ni Asasi Binafsi (54), Serikali za Mitaa - TAMISEMI (51), Polisi (18), Mahakama (15), Vyama vya siasa (06), Wizara ya Ardhi (05), DAWASA (4), NSSF (03), Taasisi za dini (02), TFF (02), Elimu ya juu (02) na Idara nyingine za TANROADS, MSD,Wizara ya Viwanda na Biashara, TADB, NMB, TRA, JIJI, TANESCO, Jeshi la Magereza, DART, TBA na TAFIRI zilikuwa na lalamiko moja moja.

Naomba nichukue fursa hii kuwapa taarifa wananchi kuwa leo tarehe 9/01/2020 tunatarajia kumfikisha mahakamani ndg AMON JOSEPH (30) mkazi wa Bunju na mtumishi wa Kinondoni football association (KIFA) kwa kosa la kuomba rushwa ya shilingi 500,000 na kupokea shilingi 330,000 kinyume na kifungu cha 15 (1) a cha sheria ya Kuzuia na kupambana na Rushwa namba 11/2007.

Ilidaiwa kuwa mnamo tarehe 18/11/2019 mtuhumiwa aliomba rushwa ya shilingi 500,000 ili aipitishe timu ya Ndwumbwi kucheza ligi ya daraja la tatu kinyume cha utaratibu na sheria. Hivyo mlalamikaji alifika ofisi za TAKUKURU Kinondoni na kutoa taarifa ambapo uchunguzi ulianza na kubaini kuwa tuhuma hizo ni za kweli, hivyo mtego wa rushwa uliandaliwa na kufanikisha kumkamata mtuhumiwa mnamo tarehe 03/01/2020 akiwa amepokea shilingi 330,000.
Uchunguzi wa Tuhuma hizi umekamilika na mtuhumiwa anafikishwa katika mahakama ya wilaya ya Kinondoni kujibu tuhuma zinazomkabili.

Ndg wana habari, mtakumbuka pia kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja kulikuwa na malalamiko ya ndg LISTON KATABAZI mkufunzi wa kujitegemea katika mchezo wa mpira wa miguu ambaye amekuwa akiibua vipaji vya vijana katika mchezo huo. Katika malalamiko yake ambayo aliyatoa kupitia vyombo mbalimbali vya habari alidai kuwa alimfundisha kijana PAUL PETER na kumwezesha kujulikana na hata kuonekana kwa uongozi wa timu ya AZAM. Lakini timu ya AZAM imemchukua kijana huyu bila kumlipa gharama zake alizoingia wakati aanaampa mafunzo ya mpira. Taarifa hizi zilifika TAKUKURU mkoa wa KINONDONI ambayo ilifuatilia na kubaini kuwa ni kweli kijana PAUL PETER aliendelezwa na Ndg LISTON KATABAZI na katika kufanya hivyo aliingia gharama mbalimbali ingawa hakuwa na nyaraka za kuthibitisha hilo. Hivyo TAKUKURU (M) wa Kinondoni uliwataka uongozi wa AZAM kukaa chini na ndg LISTON KATABAZI ili kuona njia bora ya kumaliza tatizo hilo.
Nachukua fursa hii kuwafahamisha kuwa suala hili lilipata suluhisho kwa mhusika kulipwa na ndg Katabazi ambaye siku ya leo tunaye hapa atathibitisha hilo.

Napenda kuwaasa vyama vya michezo vyote,vilabu,wachezaji,viongozi, makocha, marefa na mashabiki wote kuzingatia vigezo, taratibu n sheria katika kuendesha vyama vya michezo na michezo nchini ili tuweze kupata timu bora zitakazocheza kwa ufanisi katika mashindano hapa nchini na hata katika mashindano ya kimataifa. Nawaasa wajiepushe kabisa na vitendo vya rushwa kawa vile rushwa inapofusha na tukiiendekeza nchi yetu itaendelea kuwa kichwa cha mwendawazimu katika mashindano ya kiataifa kama mh. Rais Mstaafu ALLY HASSAN MWINYI alivyobainisha na hivyo kushusha hadhi ya nchi yetu.

MIPANGO YA MIEZI MITATU IJAYO

TAKUKURU (M) KINONDONI itaendelea na majukumu yake ya kuelimisha umma, kuchunguza, kufanya utafiti na udhibiti pamoja na kufuatilia miradi ya maendeleo. Katika kutekeleza majukumu haya TAKUKURU (M) Kinondoni imeweka mikakati maalum ya kuhakikisha elimu inaendelea kutolewa kwa wananchi na mkazo utaelekezwa katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwaka 2020.

Pia mkazo utaendelea kuwekwa kwenye uelimishaji wa wanafunzi wa Shule za Msingi, Sekondari na wanavyuo ili kuimarisha maadili kama njia ya kudhibiti rushwa ya ngono ambayo imekuwa changamoto kubwa katika Taasisi hizo.

Kwa upande wa utafiti na udhibiti mkazo utaelekezwa katika kudhibiti mianya ya rushwa katika Sekta ya Elimu,maji, ujenzi wa miundombinu, uwezeshaji viwanda, manunuzi ya umma na ukusanyaji mapato ya serikali. Kufanikisha hilo tutahakikisha miradi yote katika sekta hizi inayotekelezwa ndani ya Mkoa wa Kinondoni (Manispaa ya Kinondoni na Ubungo) inafuatiliwa katika hatua zote kwa lengo la kubaini na kudhibiti mianya ya rushwa na kuhakikisha miradi husika inakamilika kwa wakati, kwa ubora na kwa thamani halisi ya miradi hiyo.

Kwa upande wa uchunguzi,TAKUKURU (M) Kinondoni itajikita zaidi katika chunguzi zinazohusiana na vyama vaya kuweka na kukopa (SACCOS) ili kudhibiti wimbi la ubadhirifu na matumizi mabaya vya mali za vyama hivi.

Nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi na vyombo vya habari vyote kwa ushirikiano mliouonyesha kwa TAKUKURU Kinondoni kwa kipindi kilichopita.

Natoa wito kwa wananchi wote kuendelea kushirikiana nasi katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa njia mbalimbali iliwemo kufika ofisini au kwa kupiga simu TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni kupitia namba 0652 409 165 au kupiga simu au kutuma ujumbe mfupi kwenye namba 113 ambayo ni namba ya bure au kupitia TAKUKURU App inayotokana na kampeni ya UTATU.

IMETOLEWA NA:
T. MNJAGIRA
MKUU WA TAKUKURU
MKOA WA KINONDONI